**JAMU HURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KILIMO**

Anuani ya Simu "Ushirika"
Simu: +255 26- 23 22456
Telefax: +255 26- 23 21973
B.Pepe: ushirika@ushirika.go.tz

Tume ya Maendeleo ya Ushirika
Mtaa wa Kuu,
S. L. P 201
**DODOMA.**

Unapojibu tafadhali taja:

**Kumb. Na. LA.93/288/01/41** **15 Agosti, 2019**

Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi za Vyama vya Ushirika,
**TANZANIA BARA.**

Yah: **WARAKA WA MRAJIS NA. 3 WA MWAKA 2019 KUHUSU MAREKEBISHO NA UFAFANUZI WA BAADHI YA VIPENGELE VILIVYO KATIKA WARAKA WA MRAJIS NA. 4 WA MWAKA 2018**

## 1.0 UTANGULIZI

Mrajis wa Vyama vya Ushirika mnamo tarehe 25/07/2018 alitoa Waraka Na. 4 wa mwaka 2018 kwenu wenye Kumb. Na. LA. 93/288/01/33 uliohusu "***Mabadiliko ya michango ya Ada mbalimbali zinachangwa na Vyama vya Ushirika katika Mfuko wa Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika".***

Katika Waraka huo pamoja na masuala mengine, yametengwa makundi mbalimbali ya Vyama vya Ushirika ambayo yamepangiwa viwango vya malipo ya Ada kulingana na vigezo vilivyowekwa. Hata hivyo, baada ya kufanyika kwa utekelezaji wa Waraka huo pamoja na tahmini iliyofanyika kutolea ufafanuzi kwa baadhi ya maeneo na marekebisho kwa maeneo mengine.

## 2.0 MAREKEBISHO NA UFAFANUZI KWA BAADHI YA VIPENGELE

2.1 Katika kipengele 3.1 (10) cha Waraka huo, kundi ambalo linahusu michango kwa Vyama vya aina mbalimbali vikiwemo Vyama vya Ushirika wa Pamba ambapo Ada ya Mfuko wa Ukaguzi inayopaswa kuchangiwa ni Shilingi 0.5 kwa kila kilo ya zao, baada ya kikao cha wadau kilichofanyika mwezi Mei, 2019 na kuongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeelekezwa kuwa katika Msimu wa 2019/2020, makato hayo hayatafanyika, kutoka shilingi 50 kwa

kilo inayolipwa na mnunuzi kwa ajili ya gharama za uendeshaji. Aidha, mazao mengine yataendelea kuchanga kulingana na viwango vilivyopangwa au shilingi 300,000/= kwa mwaka yoyote iliyokubwa.

2.2 Katika kipengele cha 3.1 (12) cha Waraka huo, kundi linalohusu michango kwa Vyama vya aina mbalimbali vikiwemo vinavyojishughulisha na mazao mchanganyiko likiwemo zao la Miwa. Kundi hilo linalotakiwa kuchanga kiasi cha Shilingi 0.5 kwa kila kilo ya mazao. Baada ya kufanya uchambuzi, kwa sasa zao la Miwa chama hakitakatwa kwa kilo bali Tsh. 25 kwa kila Tani ya Miwa.

2.3 Katika kipengele cha 3.1 (24) cha Waraka huo, kundi linalohusu Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS), ni kwamba kwa sasa viwango vitabaki kama ilivyoelekezwa katika Waraka tajwa lakini kutoka na kuwepo kwa Sheria ya Huduma Ndogo za Kifedha na Kanuni zake pindi itakapoanza kutumika, viwango vitakavyoainishwa ndivyo vitakavyozingatiwa.

2.4 Aidha, Kipengele cha 3.2 (32) cha Waraka huo, eneo linalohusu utaratibu wa uchangiaji Elimu na Mafunzo kwa Vyama vya Ushirika baada ya kuona suala hili kutoeleweka vema, hatuna budi kutoa ufafanuzi ufuatao:-

Kwa mujibu wa Kanuni Na. 69 (1) ya Kanuni za Vyama vya Ushirika za mwaka 2015, Vyama vya Ushirika hutakiwa kutenga asilimia 10 (10%) ya mapato ghafi kwa ajili ya kuwezesha Viongozi wa Bodi, Wanachama pamoja na Watendaji wake kupatiwa elimu ya Ushirika na Mafunzo kwa vitendo. Aidha, baada ya kuona changamoto ya utekelezaji wake, Tume iliona kuna haja ya kuratibu utoaji wa mafunzo hayo kwa Vyama vya Ushirika. Hivyo, katika kutekeleza wake kila Chama cha Ushirika kitapaswa kuchangia asilimia tano (5%) ya tengo hilo kwa mwaka, kwa maana ya ((Y x 10%) x 5%) na kuingiza katika Akaunti ya Mfuko wa Ukaguzi na Usimamizi kabla ya kuidhinishiwa makisio ya mapato na matumizi ya mwaka au msimu unaofuata. Kimsingi, kiasi hicho cha fedha zitakazopatikana zitatumika kwa ajili ya kuratibu shughuli zote za mafunzo kwa wanachama, Bodi za Uongozi wa Vyama pamoja na Watendaji wake ikiwa ni pamoja na kugharamia uwezeshaji na upatikanaji wa vifaa vya mafunzo. Aidha, michango hii itagharamia shughuli za utafiti katika sekta ya Ushirika kwa ujumla.

## 3.0 HITIMISHO

Marekebisho na ufafanuzi wa baadhi ya vipengele vilivyo katika Waraka wa Mrajis Na. 4 wa mwaka 2018 utaanza kutumika rasmi kuanzia tarehe 15.08.2019. Hivyo, wahusika wote mnapaswa kuzingatia suala hilo na kinyume chake ni uvunjifu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013. Aidha, vipengele vingine vyote vinabaki kama ilivyo katika Waraka wangu Namba 4 wa mwaka 2018.

Nawatakieni utekelezaji mwema.

Tito B. Haule
**KAIMU MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA**

**Nakala**: Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb),
Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,
S.L.P. 980,
**DODOMA.**

“ Mhe. Japhet Hasunga (Mb),
Waziri wa Kilimo,
Kilimo IV Dodoma,
S.L.P. 2182,
**40487 DODOMA.**

“ Katibu Mkuu,
Wizara ya Kilimo,
Kilimo IV Dodoma,
S.L.P. 2182,
**40487 DODOMA.**

“ Mkurugenzi Mkuu,
COASCO,
S.L.P. 761,
**DODOMA.**

“ Warajis Wasaidizi wa Vyama vya Ushirika,
**TANZANIA BARA**

“ Maafisa Ushirika wote,
**TANZANIA BARA**

“ Watendaji Wakuu wa Vyama Vya Upili na Kati,
**TANZANIA BARA**

“ Katibu Mtendaji,
Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (TFC),
S.L.P. 2567,
**DAR ES SALAAM**

“ Katibu Mtendaji,
SCCULT (1992) Ltd,
S.L.P. 20640,
**DAR ES SALAAM** - **(*Kwa hatua za usimamizi*)**